

**NENO LA MKUU WA MKOA WA KATAVI MHE.
MWANAMVUA HOZA MRINDOKO WAKATI WA UZINDUZI
WA KAMATI YA USHAURI WA KISHERIA MKOA WA
KATAVI NA KLINIKI YA SHERIA YA BURE TAREHE 08
SEPTEMBER 2026**

- Mhe. Hamza S. Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
- Katibu Tawala Mkoa wa Katavi,
- Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa,
- Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Katavi,
- Wahe. Wakuu wa Wilaya,
- Makatibu Tawala wa Wilaya,
- Wakurugenzi wa Halmashauri,
- Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
- Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri Mkoa,
- Wajumbe wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa na Wajumbe wa Kamati za Ushauri za Wilaya mliopo,
- Mawakili wa Serikali na wa kujitegemea wa Mkoa wa Katavi mliopo,
- Wageni Waalikwa,
- Wanahabari,
- Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo, pilinamshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na ofisi yake na Kamati ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa wa Katavi kwa kushirikiana na Ofisi yangu katika kufanikisha sherehe hii ya uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria na Kliniki ya Sheria kwa ajili kutoa Ushauri wa Kisheria bure kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi na wilaya zake.

Ninapenda pia kuwakaribisha wageni wote mliotoka nje ya Mkoa huu. Karibuni sana Katavi.

Aidha, ninapenda pia kumpongeza Katibu Tawala pamoja na Sekretarieti ya Mkoa kwa maandalizi mazuri na kufanikisha tukio hili la leo na la kihistoria.

Ndugu Wajumbe na Wananchi,

Ninapenda kutumia fursa hii kutambua juhudi na mchango wa Kamati hizi iwapo mtakwenda kutimiza majukumu yenu itasaidia kupunguza mashauri dhidi ya Serikali na kuchochea shughuli za uwekezaji na maendeleo na pia, itaongeza utengamano katika jamii.

Ninapenda sote tuelewe kuwa jukumu la kutatua migogoro katika maisha ya Watanzania siyo la Serikali pekee, bali ni jukumu la wadau wote wa maendeleo. Kazi kubwa Serikali iliyonayo ni pamoja na kutengeneza mazingira mazuri yanayoweza kusaidia Kamati hizi za Ushauri wa Kisheria na nyinginezo kuendelea kuwepo kwa manufaa ya Watanzania wote.

Kutokana na uwepo wa Migogoro mingi katika jamii, Kamati hizi zinatakiwa kukaa kila mara kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya kusikiliza malalamiko ya kisheria na kutoa elimu kwa umma kwa kushirikiana na ofisi yangu na ofisi za Wakuu wa Wilaya. Kuna Kamati nyingi ambazo zote zinalenga kutatua matatizo ya wananchi, ninapenda kutoa rai kwenu kuwa ipo haja ya kuhakikisha kuwa Kamati hii ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa na zile za Wilaya zinafanya mambo yafuatayo ili kukabiliana na migogoro iliyopo:-

- i. Kuendelea kuboresha kiwango cha utoaji wa huduma ya ushauri wa kisheria na kuongeza wigo na upatikanaji wenu katika maeneo ambayo hayajafanikiwa kufikiwa hasa maeneo ya vijijini.
- ii. Kujiwekea utaratibu wa kuandaa Kliniki za Kisheria kwa utaratibu wa kuwafuata wananchi katika maeneo yao. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, wapo wananchi ambao wanaogopa kuingia kwenye ofisi za serikali na wengine hawana uwezo wa kusafiri na kwenda katika ofisi hizo.
- iii. Pia, kuhakikisha mnapopokea malalamiko au migogoro mnaifuatilia mpaka mwisho wake ili kujiridhisha ni namna gani imemalizika na kuweka kumbukumbu ya kufungua na kufunga migogoro hiyo. Lengo ni kuzuia walalamikaji kurudi baadaye kurudia kuwasilisha malalamiko yaliyopita hasa pale anapoona uongozi umebadilika.
- iv. Zoezi la kutoa elimu kwa umma ni endelevu na siyo lazima lisubiri kamati. Iwapo huduma hiyo itahitajika katika

maeneo yenu ya kazi, muwe tayari kutoa elimu ya kisheria kwa viongozi, watumishi wa umma na wananchi kwani idadi kubwa ya wananchi wetu bado hawajui mambo ya kisheria na pia hawajui wapi waende au nini cha kufanya iwapo watapata shida.

Ndugu Wajumbe na Wananchi;

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, ninapenda kutumia nafasi hii kuielekeza Kamati za Ushauri wa Kisheria ya Mkoa, Kamati za Ushauri wa Kisheria za Wilaya na wadau kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuwahudumia Wananchi. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kamati ya Ushauri wa Kisheria kwa kushirikiana na Ofisi yangu, zimeonyesha mfano mzuri wa ushirikiano kwa kutoa huduma za ushauri wa kisheria ndani ya Mkoa wa Katavi. Kwa niaba ya Serikali ya Mkoa, ninapenda kuwahakikishia kuwa, Serikali itaendelea kuwaunga mkono katika juhudi zenu za kuwasaidia Watanzania.

Mwisho, ninapenda kwa mara nyingine tena kumshukuru Katibu Tawala wa Mkoa na Sekretarieti ya Mkoa kwa ujumla kwa kuwaalika katika shughuli hii. Pia, ninawashukuru sana Kamati kwa maandalizi mazuri. Nimefarijika sana na ninawatakia kila la kheri katika kufanikisha malengo na mipango mliyojiwekea.

Baada ya kusema haya, sasa ninaomba kumkaribisha Mhe. Hamza S. Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa hotuba yake na kufanya uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ya Mkoa pamoja na zile za Wilaya za Kliniki ya Sheria ya bila malipo kwa Mkoa wa Katavi.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Katavi.

"Asanteni sana kwa kunisikiliza"